



Maelezo ya Jumla ya Australia

Lugha

English

Kiingereza ni lugha ya kitaifa ya Australia.



Kujifunza jinsi ya kuzungumza Kiingereza ni muhimu sana unapoishi Australia.



Watu wengine nchini Australia huzungumza lugha zingine pia.

200+

Zaidi ya lugha 200 zinasemwa katika:

- nyumba
- jamaa – vikundi vya watu waliounganishwa



Hii ni kwa sababu karibu watu 25% wanaoishi Australia walizaliwa katika nchi nyingine.



Pia kuna lugha zaidi ya 20 zilizosemjiwa na Watu wa asili na wa Visiwa vya Torres Strait.

Tunaita hizi lugha za asili.

Watu wa asili wa Australia



Watu wa Asilil na wa Visiwani vya Torres Strait wamekuwa wakiishi Australia kwa karibu miaka 50,000.


Pia tunawaita watu wa asili.



Wana mojawapo ya tamaduni za zamani zaidi ulimwenguni.



Kuna Watu wa Asili na wa Visiwani vya Torres Strait Islander wanaoishi katika kila jimbo na wilaya ya Australia.




Katika sehemu mbalimbali za Australia, Watu wa Asili na wa Visiwani vya Torres Strait wana tofauti:

- lugha



- imani ya utamaduni



- imani ya kiroho

Australia ya utamaduni mwingi



Watu wanahamia Australia kutoka duniani kote.

Tunawaita watu hawa wahamiaji.



Zaidi ya watu milioni 7.5 wamehamia Australia tangu 1945.



Wahamiaji zaidi wa 800,000 wamekuwa wakimbizi.



Wakimbizi ni watu wanaohitaji kuondoka nyumbani kwao kwa sababu hawana Usalama tena.


1/2

Karibia nusu ya Waaustralia wote walikuwa:

- walizaliwa ng'ambo
- wana mzazi aliyezaliwa nchi ya ng'ambo



Hii hufanya Australia mahali palipo na utamaduni mwingi.



Australia haina dini rasmi au dini ya taifa.



Wewe upo huru kufuata dini unayochagua wewe.



Dini yako huhitaji kuelewana na jinsi sheria zinavyosema.



Hii ikiwemo ni pamoja na sheria:

- kwa Waaustralia wote – sheria za Jumuyia ya Serikali
- sheria za nchi na wilaya



Waaustralia wanaunganishwa kwa njia ya maadili yao.



Maadili ni mambo ya Waaustralia wote wanaoamini ni muhimu:

- usawa – kila mtu hutendewa sawa na ana haki sawa



- demokrasia – kila mtu anaweza kuhusika katika jinsi nchi inavyo ongozwa



- uhuru



- heshima kwa wote

